

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA NZEGA ("NZEGA WSSA") KWA MWAKA 2017/18 – 2019/20

Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR--W-17-09

Mnamo tarehe 12 Juni 2017, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega (Nzega WSSA) la kutaka kuongeza bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2017/18 hadi 2019/20. Jedwali namba 1 hadi 6 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za za Maji sasa na zinazopendekezwa (shilingi kwa mita moja ya ujazo)

Aina za wateja	Bei za sasa	Bei zilizopendekezwa					
	2016/17	% Ongezeko	2017/18	% Ongezeko	2018/19	% Ongezeko	2019/20
Majumbani	750	63%	1,222	6%	1,295	8%	1,404
Biashara	930	113%	1,978	6%	2,096	8%	2,273
Taasisi	860	64%	1,411	6%	1,495	8%	1,621
Viwandani	0	NA	1,978	6%	2,096	8%	2,273
Magati	1000	110%	2,104	6%	2,229	8%	2,418
Mabirika ya kunyweshea mifugo	3,757	4%	3,906	6%	4,139	8%	4,488

Jedwali 2: Gharama ya Huduma ya Sasa na Iliyopendekezwa (shilingi/mwezi)

Aina za wateja	Bei za sasa	Bei zilizopendekezwa					
	2016/17	% Ongezeko	2017/18	% Ongezeko	2018/19	% Ongezeko	2019/20
Majumbani	500	300%	2,000	0%	2,000	500	300%
Biashara	1000	150%	2,500	0%	2,500	1000	150%
Taasisi	1000	150%	2,500	0%	2,500	1000	150%
Viwandani	1000	150%	2,500	0%	2,500	1000	150%

Jedwali 3: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya (Shilingi kwa maunganisho mapya)

Aina za wateja	Bei za sasa		Bei zilizopendekezwa
	2016/17	% Ongezeko	2017/18-2019/20
Majumbani	15,000	33%	20,000
Biashara	17,000	47%	25,000
Taasisi	17,000	47%	25,000
Viwanda	0	NA	25,000

Jedwali 4: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshwa Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwa marejesho)

Aina za Wateja	Bei za sasa	Bei zilizopendekezwa			
	2016/17	% Ongezeko	2017/18	% Ongezeko	2018/19- 2019/20
Majumbani	10,500	43%	15,000	0%	15,000
Biashara	11,000	45%	16,000	0%	16,000
Taasisi	11,000	36%	15,000	7%	16,000
Viwanda	0	NA	16,000	0%	16,000

Jedwali 5: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Mita ya Maji kwa Mteja (Shilingi kwa mwezi)

Aina za wateja	Bei za sasa		Bei zilizopendekezwa
	2016/17	% Ongezeko	2017/18-2019/20
Majumbani	500	200%	1,500
Biashara	500	200%	1,500
Taasisi	500	200%	1,500
Viwanda	0	NA	1,500

Jedwali 6: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Fomu ya Maombi ya Kujiunga na Huduma ya Maji kwa Mteja Mpya (shilingi/fomu)

Aina za wateja	Bei za sasa		Bei zilizopendekezwa
	2016/17	% Ongezeko	2017/18-2019/20
Majumbani	5000	0%	5000
Biashara	5000	0%	5000
Taasisi	5000	0%	5000
Viwanda	5000	0%	5000

Kutokana na wasilisho la Nzega WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Nzega WSSA kuongeza mapato ili kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo, kupanua mtandao wa usambazaji majisafi kwenye makazi mapya na kuweza kupata fedha ya kulipia uchakavu wa miundombinu ya majisafi .

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 28 Septemba, 2017 katika Ukumbi wa FDC Kitongo, Nzega Mjini** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni

ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu ndani ya kipindi kabla ya tarehe **6 Oktoba, 2017**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi ya EWURA, **GHOROFA YA SABA, LAPF PENSIONS FUND TOWER; MKABALA NA KIJIKI CHA MAKUMBUSHO, KIJITONYAMA, DAR ES SALAAM** au ofisi za Nzega WSSA zilizoko mjini Nzega.

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
6 Septemba 2017